JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA UCHUKUZI

MAMLAKA YA UDHIBITI USAFIRI ARDHINI

# TAARIFA KWA UMMA

## ONYO KWA WATOA HUDUMA WATAKAOKIUKA MASHARTI YA LESENI ZA USAFIRISHAJI ABIRIA MIJINI (DALADALA)

Mamlaka imebaini uwepo wa baadhi ya watoa huduma za usafiri wa abiria mijini (daladala) waliokusudia kupandisha nauli za usafiri huo kiholela kwa madai ya kupanda kwa bei ya mafuta (diseli na petrol). Pamoja na LATRA kukutana na watoa huduma hao kwa kuwaelimisha juu ya utaratibu unaopasa kufuatwa kisheria, baadhi yao wameonesha nia ya wazi kupinga na wamekusudia kukiuka masharti ya leseni zao kwa kupandisha nauli kiholela. Azma hii ovu haikubaliki katika Nchi yetu hasa kipindi hiki ambacho, Serikali yetu sikivu kupitia LATRA, imeanza kushughulikia maombi ya kufanya marejeo ya nauli.

Kwa mujibu wa kanuni ya 30 ya Kanuni za Leseni za Usafirishaji (Mabasi ya Abiria) za Mwaka 2020 (Tangazo la Serikali Na. 76 la tarehe 7/2/2020), ni kosa kutoza nauli zaidi ya kiwango kilichoidhinishwa na Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA). Amri ya LATRA iliyotangazwa kwenye Gazeti la Serikali Na. 8 la tarehe 6 Mei, 2022, iliweka viwango vya nauli kwa mabasi ya mijini (daladala), ambavyo bado havijabadilika, kama ifuatavyo:

| Na. | Umbali (Kilometa) | Nauli (Sh.) |
|---|---|---|
| 1. | Zisizozidi 10 | 500 |
| 2. | Kati ya 11 na 15 | 550 |
| 3. | Kati ya 16 na 20 | 600 |
| 4. | Kati ya 21 na 25 | 700 |
| 5. | Kati ya 26 na 30 | 850 |
| 6. | Kati ya 31 na 35 | 1,000 |
| 7. | Kati ya 36 na 40 | 1,100 |
| 8. | Nauli ya mwanafunzi | 200 |

Hivyo, Mamlaka inawatahadharisha watoa huduma waliokusudia kujipangia na kujitangazia nauli kinyume cha Sheria na Kanuni za Usafirishaji wasitishe kusudio lao na wasubiri matokeo ya mchakato unaoendelea wa kufanya marejeo ya nauli hizi.

Mamlaka itaendelea kutoa elimu kwa umma na haitasita kuchukua hatua stahiki kwa mtoa huduma yeyote au kundi la watoa huduma watakaobainika kukiuka masharti ya leseni zao.

*Imetolewa na:*

CPA. Habibu J. S. Suluo

**MKURUGENZI MKUU**

16 Oktoba, 2023